HOTUBA YA MHE. ENG. EVARIST NDIKILO, MKUU WA MKOA WA PWANI KWENYE HAFLA YA UFUNGUZI WA MNADA WA KOROSHO MSIMU WA MWAKA 2020/ 2021 WILAYANI KIBITI
TAREHE11 NOVEMBA, 2020

Mhe. Gullamhussein Kifu, Mkuu wa Wilaya ya Kibiti,

Ndugu Shangwe Twamala - Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Pwani,

Wah. Wakuu wa Wilaya - Rufiji, Kisarawe, Mkuranga na Kibaha,

Wakurugenzi wa Halmashauri, Kibiti, (Mr. Mavura)

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Korosho Tanzania,

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa Soko la Bidhaa Tanzania,

Mwakilishi wa Mwenyekiti - CORECU Ltd,

Wataalam na Watendaji ngazi ya Mkoa na Halmashauri,

Wanunuzi wa Korosho,

Wenyeviti na Makatibu wote wa AMCOS,

Wakulima wa Korosho,

Waandishi wa habari,

Mabibi na Mabwana.

Ndugu Wadau;

Awali ya yote nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima uliotuwezesha kukutana hapa tukiwa wenye afya njema.

Pili, napenda kuwapongeza na kuwashukuru sana Wakulima wa Korosho na Wadau wote wa Tasnia ya Korosho Mkoani Pwani kwa ushirikiano mkubwa mnaouonesha kwenye mchakato huu wa ukusanyaji wa Korosho hadi kuzifikisha ghalani na leo zimeingia kwenye Mnada wa Kwanza wa Mauzo. Nasema hivyo kwa sababu uvunaji wa Korosho hadi leo tunaziona ghalani ni mchakato unaohitaji kila mdau, kuanzia Wakulima, AMCOS,

Chama Kikuu, Wasafirishaji, Waendesha Maghala na Taasisi za Serikali kujipanga na kuwa na ushirikiano wa hali ya juu. Kwa hiyo hongereni sana Wadau kwa ushirikiano huo.

Ndugu Wadau;

Leo tumekutana hapa kuzindua rasmi Minada ya uuzaji wa Korosho, kufuatia Mkutano wa Wadau uliofanyika tarehe 13 Oktoba, 2020 pale Wilayani Mkuranga. Katika mkutano ule ambao karibu Wadau wote wakiwemo Wakulima na Wanaushirika waliwakilishwa vizuri, tulijadili masuala mengi ikiwamo Maandalizi ya Ukusanyaji na Uuzaji wa Korosho Msimu huu wa 2020/2021. Miongoni mwa masuala yaliyojadiliwa kwa kina sana kama sehemu ya maandalizi ilikuwa ni Upatikanaji wa maghala makuu, Upatikanaji na usambazaji wa magunia, Maandalizi ya Mizani, Maandalizi ya magari kwa ajili ya kusafirishia Korosho kutoka kwenye maghala ya AMCOS kwenda kwenye maghala makuu na uwepo wa Nyaraka muhimu za kukusanyia na kusafirshia Korosho. Lakini juu ya yote, tulijadili kuhusu Ubora wa Korosho zetu kwa kuwa ndiyo kigezo muhimu cha upatikanaji na bei nzuri kwa wakulima.

Ndugu Wadau ;

Nimeambiwa, masuala yote tuliyokubaliana yameendelea kufanyiwa kazi na kutuwezesha kuanza minada siku ya leo, tarehe 11 Novemba, 2020. Napenda kuwashukuru kila mmoja kwa nafasi yake kwa kutekeleza majukumu tuliyopangiana. Pamoja na pongezi hizo nimeambiwa kuna changamoto bado zipo, hasa upatikanaji wa magunia katika baadhi ya Wilaya, hasa hapa Kibiti, upatikanaji wa ghala kuu hasa kule Kibaha na ubora wa Korosho katika baadhi ya maeneo.

Nimeagiza na hapa ninaagiza changamoto zote zilizosalia ziendelee kufanyiwa kazi kadri tunavyoendelea na msimu. Upatikanaji wa magunia ni suala muhimu na CORECU mnatakiwa kufanya kazi usiku na mchana kuhakikisha Mzabuni analeta magunia ya kutosha na kwa wakati na ninyi kuyasambaza kwa wakati kwenye AMCOS zote. Kama tulivyokubaliana, magunia hayo yasigawiwe kwa wakulima na kuyapeleka majumbani bali mkulima ayakute kwenye ghala la AMCOS. Hii itasaidia kudhibiti gharama za mahitaji ya magunia na pia kudhibiti ubora kwani baadhi ya wakulima wanakuwa siyo waaminifu kwa kuchanganya Korosho na vitu vingine kama mawe, mchanga na hata matofari ili kuongeza uzito.

Wakati suala la ghala kuu kule Kibaha linatafutiwa ufumbuzi, hivyo Korosho za wakulima wa Kisarawe, Kibaha, Bagamoyo na Chalinze ziendelee kukusanywa na tuhakikishe zinaingia kwenye mnada ujao.

Ubora wa Korosho kama nilivyosema bado ni changamoto, ikizingatiwa kwamba mvua zimeanza kunyesha katika maeneo mengi ya Mkoa wetu. Kwa hiyo wakulima tujitahidi kuanika na kudarajisha Korosho zetu katika hali hiyohiyo tuliyonayo. Korosho zinazoshindwa kupata vigezo vya kupokelewa ghala kuu zichambuliwe vizuri na AMCOS husika na siyo kuchanganywa na nzuri.

Ndugu Wadau ;

Tunapoanza rasmi zoezi la uuzaji wa Korosho kupitia minada, yapo masuala muhimu yanayotakiwa kutekelezwa na wahusika wote bila visingizio, kama ifuatavyo :-.

(i) Viongozi wote katika ngazi zote simamieni zoezi la ukusanyaji wa Korosho na kuhakikisha kwamba korosho zote zinaelekezwa kwenye mfumo rasmi wa stakabadhi mazao ghalani. Njia nyingine nje ya mfumo huu, siyo rasmi na haziruhusiwi. Hili liende sambamba na udhibiti wa Korosho zinazotolewa nje ya Mkoa na Halmashauri zetu kinyume cha utaratibu, hali inayosababisha Halmashauri na Vyama vya Ushirika kukosa ushuru wao.

(ii) Viongozi wa Vyama vya Msingi vya Ushirika (AMCOS) hasa Makatibu kuweni makini sana kwa kujiepusha kabisa na ubadhilifu wa korosho za wakulima wenzenu. Orodha za wakulima walioleta Korosho na kilo zao ziwekwe wazi na malipo yanayotolewa yaendane kwa uwazi na jina na kiasi cha Korosho kilichokusanywa. Korosho zipokelewe na kutunzwa vizuri maghalani. Upotevu wa makusudi wa korosho kwa visingizio vya unyaufu haukubaliki na wahusika wote watawajibika. Vitabu vya stakabadhi vitakavyotumika kukusanyia korosho ni vile vilivyotolewa na Chama Kikuu cha Ushirika (CORECU) kwa ajili ya matumizi ya msimu huu na si vinginevyo.

(iii) Wakulima waendelee kuboresha ubora wa korosho zao. Katika kutekeleza hilo, waendelee kuanika na kudarajisha korosho zao. Baadhi ya wakulima walirejeshewa Korosho mwaka jana kwa malengo ya kubangua. Nawaomba wajiepushe kuchanganya korosho hizo na za msimu huu kwani haikubaliki na ni kinyume cha utaratibu ili kuendelea kulinda heshima na soko la zao letu.

(iv) **Taratibu zote za minada zifuatwe:** na leo tutashuhudia hapa kulingana na Mwongozo uliotolewa na Bodi ya Korosho Tanzania na kukubaliwa kwenye Mkutano wa Wadau. Baada ya mnada, walioshinda zabuni wafanye malipo ndani ya siku nne (4) za kazi, kuondoa korosho zao kwenye maghala ndani ya siku saba (7) za kazi na Wakulima walipwe fedha zao ndani ya siku 10 za kazi. Yeyote atakayevunja au kukiuka utaratibu hatavumiliwa hata kidogo.

(v) Makato yote yaliyokubaliwa na Wadau ngazi ya Taifa na Mkoa yafanyike kwa mujibu wa makubaliano. Makato nje ya yaliyokubaliwa hayataruhusiwa.

(vi) Usafirishaji wa korosho kutoka kwenye maghala ya AMCOS kwenda kwenye maghala makuu na maghala makuu kwenda bandarini, maghala ya wanunuzi au viwandani ni lazima ufuate utaratibu uliokubalika, yaani kuanzia saa 12 asubuhi hadi saa 12 jioni na Korosho zote ziambatane na nyaraka husika.

(vii) Wahe. Wakuu wa Wilaya tuwahimize TARURA kufuatilia hali ya barabara zinazokwenda kwenye maeneo yenye Korosho ili iwe rahisi kuzihamisha kutoka kwenye maeneo hayo.

(viii) Baada ya mauzo na malipo kufanyika, CORECU na AMCOS ambao ndiyo wakusanyaji wa ushuru mbalimbali kwa niaba ya

wadau wengine kwenye mnyororo wa thamani wawasilishe fedha hizo kwa wakati.

(ix) Chama Kikuu cha Ushirika (CORECU) na AMCOS mhakikishe wakulima wanalipwa kwa wakati na kikamilifu. Aidha, Wakulima wote wanapaswa kuwa na akaunti benki na kuhakikisha Jina la mkulima aliyekusanya korosho linaendana na jina la akaunti ya benki ili kuondoa usumbufu na ucheleweshaji wa malipo.

Ndugu Wadau ;

Mwisho, nirudie tena kuwashukuru kwa mara nyingine kwa maandalizi na kushiriki kwenye hafla hii muhimu. Ni matumani yangu kwamba tutatekeleza yote tuliyoelekezana kulingana na majukumu ya kila mmoja wetu. Korosho ni zao muhimu sana katika maisha yetu hivyo halina budi kupewa umuhimu unaostahili.

Baada ya kusema hayo nitamke sasa kwamba Minada ya Uuzaji wa Korosho Mkoani Pwani imezinduliwa rasmi na Sasa nipo tayari kushuhudia uuzaji huo (Tani 2,073 Daraja la 1 & 2).

Asanteni sana kwa kunisikiliza.